Kupanda Kanisa



HUDUMA YA UVUVIO AUSTRALIA

KIMEANDALIWA NA
Mtume Paul Galligan

MUONGOZO KATIKA UPANZI WA KANISA

YALIYOMO

Utangulizi

Sura ya 1. Kanisa ni nini?

Sura ya 2. Kulipanda kanisa

Sura ya 3. Kulikuza kanisa

Sura ya4. Kulikamilisha kanisa

KARIBINI KATIKA MUONGOZO HUU KUHUSU UPANZI WA KANISA

MPANGO WA KULIFIKIA TAIFA

Mwishoni mwa 1998, BWANA alianza kuuchochea ufahamu wangu juu ya mpango wa kulifikia Taifa, hasa Australia. Naamini kuwa mpango huu ni kwa ulimwengu mzima kwa sababu ndivyo Maandiko Matakatifu yanavyotuagiza. Yesu aliwaamuru wafuasi wake[wanafunzi, kanisa] kuihubiri Injili kwa watu wote na kuwafanya mataifa wote kuwa wanafunzi.

KUPANDA, KUTIA MAJI, KUKUA

Po pote pale ambapo watumishi wa BWANA wanaenda katika huduma katika kutii amri Yake, wakiwa wametumwa na Roho Mtakatifu kufanya kazi ya huduma, kunakuwa na upanzi wa Kanisa, na kufariji [kutia maji] kwa kanisa kusababisha kukua, na kukamilika. Katika nyakati hizi, Mungu yuko anarejesha karama, mito na huduma kwa kanisa Lake ili **kuhubiri Injili, kuwafanya wanafunzi waaminio wengi, na kulikamilisha kanisa**, kutaendelea kulingana na mapenzi yake, kutimiza kusudi Lake la milele alilokamilisha katika Kristo Yesu.

KUTENGENEZA YALIYOPUNGUA KATIKA KANISA

Baada ya mtume Paulo na kikundi chake kufaulu kuihubiri Injili kule Krete, Paulo alimtuma Tito kurudi katika miji ambayo walikuwa wamewahubiri watu habari njema na kuwaleta Kwake Kristo, ayatengeneza yaliyo pungua katika, kuweka wazee katika kila mji. Wakati watu wanapo okoka kanisa linapandwa. Hatua inayofuata ni kuchagua uongozi, kutambua karama na mwito wa huduma ambayo Bwana ametoa kwa ajili ya Watu wa Mungu.

Makanisa, shirika, hukusanyika mahali ambapo huduma katika utano inazaa matunda na kanisa linapandwa. Ile huduma katika utano inahusika na **kuyatengeneze yaliyo pungua katika kanisa: kutoa muongozo wa kiutume**, **muongozo wa kinabii**, kuendelea **na uinjilisti** katika jumuia kwa kumuhubiri Kristo hadharani na nyumba kwa nyumba, **kulichunga kundi la Mungu** na **Kufundisha funzo la mitume kila siku**.

KANISA NI NINI?

Kanisa Lake Kristo sio vikundi vidogo vidogo[madhehebu] visivyo kuwa na uhusiano! Wala sio dini zenye ustadi na kuongozwa katika mpango wa kidini! Tena sio kujumuishwa katika kanisa la kipentekoste au kanisa la kiinjilisti! Tena sio huduma inayonawiri katika Runinga! Wala sio muungano wa ruwaza ambapo Neno La mungu limerudishwa kuwa desturi za watu ambazo zinawawekea watu mipaka Fulani!

Kanisa la Yesu Kristo halijulikani kimsingi kwa kusoma historia ya kanisa hata japo kanisa la kihistoria ijapo lilionekana kuwa lilifaulu. **Kanisa Lake Yesu Kristo linajulikana kwa ufunuo kutoka Kwa Neno la Mungu na kurudia funzo la mitume na misingi katika Neno la Mungu.** Kanisa la kweli limeposwa na Yesu Kristo, sio kwa mwanadamu Fulani mahali Fulani katika historia ya kanisa au katika huduma ya kisasa. Ni lazima tumheshimu Bibi arusi wa Yesu Kristo na tusiuharibu mpango mzuri wa Mungu.

HEKALUNI NA NYUMBA KWA NYUMBA

Kanisa la Agano Jipya lilikutana Hekaluni na nyumba kwa nyumba. Yesu Kristo na Injili Yake walihubiriwa na kufundishwa hekaluni na nyumba kwa nyumba. Katika Maandiko Matakatifu kuna makanisa katika nyumba yaliyo kutana kila siku na pia kulikuwa na huduma wazi, hekaluni, shuleni barabarani, mbele ya mabaraza au mbele ya mfalme. Tuna amrishwa kukutana katika vikundi vidogo vidogo, katika nyumba, pia tunaamrishwa kuwatuma mitume, manabii, na wainjilisti kuihubiri Injili na kupanda makanisa mapya. Kuna kutawazwa na kukuza wachungaji

na waalimu katika kulitunza kundi la Mungu. Kuna mpango mahususi wakufuatwa katika kulileta kanisa katika utimilifu: unapatikana katika Neno la Mungu.

Kupanda kanisa, kukuza kanisa, na kulikamilisha kanisa
Ni huduma ya Mungu aliyoipa kanisa.

Ni jambo la kuogopesha, la changamoto, la ajabu na la kuzawadiwa wakati ambapo tunamtumikia Kichwa cha Kanisa na Bwana wa Mavuno, Mfalme wetu ajaye, Bwana Yesu Kristo.

Sura ya 1:

Kanisa ni nini?

EKKLESIA
Kanisa:- S.C. 1577 ***'ekklesia'***, **kuitwa kutoka** [kutoka katika asili]; kidunia, **kusanyiko la watu** (**Matendo 19: 32, 39,41**); katika Kiyunani Agano la Kale. [Septuagint] kusanyiko la Israeli, kama **Matendo 7:38** ***'Kanisa'*** jangwani; jumuia ya wakristo waliowatakatifu hapa duniani au mbinguni au kwote.

YESU NA NDUGU ZAKE = KANISA
Ebr.2:12 [akinukuu kutoka **Zab.22:22**] ***"…Nitalihubiri Jina lako kwa ndugu zangu; katika kusanyiko nitakusifu."*** Mwandishi wa waraka kwa Waebrania anautumia mfano huu kuwa ni wa Yesu Kristo, ambaye anawaita washiriki wa kanisa, ***"Ndugu zangu,"*** na anasema ***"nitakusifu,*** [Yahova] ***katika kusanyiko,*** [kanisa]".

Kanisa ni wale walioitwa kutoka miongoni mwa watu, wale ambao Aliwahatimisha kugeuzwa katika mfano wa Mwana Wake, walioitwa, waliohesabiwa haki na kutukuzwa, **Rum.8:29-30.** Kanisa ni wale wasiojikwaa kwa ajili ya mafunzo Yake magumu. (**Yoh.6:60**), wanaojua uzima wa milele unapatikana katika maneno ya Bwana Yesu, (**Yoh.6:68**).
Yoh.5:24 ***"Amin, amin, nawaambia, yeye alisikiaye Neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele, wala haingiii hukumuni bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani."***

YESU YUKO ANALIJENGA KANISA

Katika **Matt.16:18** tunapata jina 'kanisa' [ekklesia] kwa mara ya kwanza. ***"Nami nakuambia, wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda."***

Yesu amejitolea katika **"kulijenga Kanisa"**. Anatangaza kuwa halitashindwa na milango ya kuzimu. Litajengwa kwa msingi wa imani ndani Yake: ***"Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai."*** **Matt.16:16-17.** Hili laweza tu kufahamika kwa njia ya ufunuo kutoka kwa Mungu, akimletea imani yule anayeamini.

JENGWA JUU YA MWAMBA
Yesu ni *"petra"* mwamba ambapo kanisa linajengwa.
1 Kor.10:4 ***"…wote wakanywa kinywaji kile kile cha Roho; kwa maana waliunywea ule mwamba wa roho uliowafuata; na mwamba ule ulikuwa ni Kristo."***
Matt.7:24-27 ***"basi kila asikiaye hayo maneno na kuyafanya, atafananishhwa na mtu mwenye akili, aliye jenga nyumba yake juu ya mwamba; mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma zikaipiga nyumba ile, isianguke; kwa maana misingi yake imewekwa juu ya Mwamba." Na kila asikiaye hayo maneno na asiyafanye, atafananishwa na mtu mpumbavu, aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga, mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma zikaipiga nyumba ile, ikaanguka;nalo angulo lake likawa kubwa.***

YESU NDIYE JIWE LA MSINGI NA PIA JIWE KUU LA PEMBENI
Kanisa ni kusanyiko la Bwana Yesu. Bwana ndiye mjenzi wa kanisa. ***Yeye ndiye msingi, jiwe lililojaribiwa, jiwe la pembeni lenye dhamani; msingi ulio imara***. **Isa.28:16**
Zab.118:22-23 ***"Jiwe walillolikataa waashi, limekuwa jiwe kuu la pembeni. Neno hili limetoka kwa BWANA ; nalo ni ajabu machoni petu."*** [nukuliwa katika **1Pet.2:7**].

YESU NI MTUME [**MJENZI**]
Yeye ni mtume ***"Aliyekuwa mwaminifu kwake yeye aliyemweka,"*** [**Ebr.3:2**]. Yesu Masihi ni mjenzi wa nyumba ya Mungu, kanisa. **Ebr.3:3** ***"Kwa maana huyo amehesabiwa kuwa amestahili utukufu zaidi kuliko Musa, kama vile yeye aitengenezaye nyumba alivyo na heshima zaidi ya hiyo nyumba.."*** Yeye ni Mwana juu ya Nyumba Yake, ***"ambaye nyumba yake ni sisi,"*** **a.6.**

Yule aliyeuweka msingi wa nyumba ya Mungu ndiye atakaye imaliza. **Zak.4:9** ***"Mikono yake Zerubabeli imeiweka misingi ya nyumba hii, na mikono yake ndiyoitakayoimaliza."*** Zerubabeli ni mfano wa Kristo, aliyetumiwa na Mungu kujenga tena hekalu la Mungu Yerusalemu baada ya uhamisho wa Babeli. Huu mstari unazungumzia kiunabii kuhusu Yesu, kama mtume wa Mungu, anajenga Kanisa.

PETRO, JIWE DOGO LA MSINGI

Petro ni *"petros"* jiwe, ambaye atakuwa jiwe la msingi kama mtume. Kanisa linajengwa na Kristo katika huduma za msingi- mitume na manabii ambao amechagua kanisani. **Efe.2:20** ***"mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Yesu Kristo mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni."*** Kila aaminiye anaitwa jiwe lililo hai na anajengwa kuwa nyumba ya Mungu, Kanisa.
1Pet.2:5 ***"Ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmejengwa mwe nyumba ya Roho, ukuhani mtakatifu, mtoe dhabihu za roho, zinazikubaliwa na Mungu kwa njia ya Yesu Kristo."***

FUNGUO ZA UFALME
Katika **Matt.16:19** Yesu anampa Petro, mtume wa msingi, funguo za ufalme wa mbinguni, ***"Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni; na lo lote utakalo lifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni; na lo lote utakalo fungua duniani litakuwa limefunguliwa mbinguni."*** Kazi ya funguo ni kufungua milango iliyokuwa imefungwa; pia zinawakilisha mamlaka.

Tutazame jinsi Petro alivyotumia hizo funguo kutimiza tume
Matendo 2:14-41 Petro anahubiri Siku ya Pentekoste. Matokeo ya ujumbe huu wa upako ni kwamba Wayahudi 3000 wakaokoka.
Matendo8:14-25 Petro na Yohana walienda Samaria, wakawaombea wanafunzi nao wakajazwa Roho Mtakatifu.
Matendo10:9-48 Petro alienda nyumbani mwa Kornelio, akaihubiri Injili na Roho Mtakatifu akawashukia Mataifa walioamini.
Matendo 3:6-9 Ishara na maajabu yakitendeka, kiwete anaponywa.
Matendo 5:3-11 Petro anahukumu dhambi ya Anania na Safira.
Matendo 9:32-35 Petro anamponya mtu aliyepooza kwa miaka nane.
Matendo 9:36-43 tabitha anafufuliwa kutoka kwa wafu.

KUFUNGA NA KUFUNGUA
Yesu anampatia Petro mamlaka ya kufunga na kufungua.

> **Matt.16:19**: Funguo zinamaanisha mamlaka. Kupitia kwake Petro, ambaye ni mwakilishi wa kanisa katika vizazi vyote. Yesu anapokeza mamlaka Yake kwa kanisa Lake kufunga na kufungua hapa duniani. "Kufungua (**Rum.6:14**). Kama kuna mtu ambaye amepagawa na pepo, 'kanisa' linaweza "kufunga" huyo pepo kwa; kuliamuru kutoka (**Matendo 16:18**), tukitambua kuwa ni Yesu alifanya hili kuwezekana (**Matt.12:29**). Jinsi kanisa linavyofungua na kufunga limo katika njia nyingi na wakati mwingine huenda hata zaidi ya kutumia haya maneno tu katika sala zetu.

MWITO WA YESU

Mwito wa Yesu ni nini? Ni kuokoka? Ni kujiunga na kanisa?

Mwito wa Yesu ni: 1. Kuwa wavuvi wa watu
2. Kuchukuwa msalaba
3. Kupoteza nafsi yako
4. kumfuata Yesu

Neno ***'Kufuata'*** SC #190: *'akoloutheo'* kuambatana, kuenda pamoja na, kuenda njia moja na, kufuata Yule aliye mbele. Kwa sababu neno lilitumiwa na wanajeshi, watumwa na wanafunzi, linaweza kutumiwa kwa njia rahisi katika maisha ya Mkristo.

5. Kuacha vitu vyote
6. Kustahimili mateso
7. Kuwa wachungaji
8. Kupokea Roho Mtakatifu
9. Kuwa shahidi
10. Kuihubiri Injili kwa Ishara na maajabu
11. Kuwafanya mataifa yote kuwa wanafunzi, kubatiza na kufundisha
12. Kujiandaa kwa kurudi Kwake
13. Kuwapokea wale Aliowatuma
14. Kuitikia mwito na kuwa mwaminifu kwa maono ya mbinguni
15. kuokoka, pamoja na ubatizo wa maji mengi
16. kuwekwa katika mwili kama kiungo
17. kuwekwa kanisani kama mhudumu
18. kuwa sehemu ya kanisa lililopandwa
19. kujiunga kikamilifu kama kiungo katika kanisa.

KUKUZA KANISA: NJIA YA BIBLIA

Usitazame desturi za mtu na njia za ulimwengu. Fuata maelezo ya Bwana Yesu na mifano kutoka kwa wanafunzi wake. Walihubiri na kufundisha katika hekalu na pia nyumba kwa nyumba. Walitangaza kuwa Yesu wa Nazareti ni Mwana wa Mungu. Walihubiri kuwa Yesu ni Masihi. Na walifaulu katika kupanda mbegu katika himaya ya kirumi na Injili ya Bwana Wetu Yesu Kristo. Hatuhitaji kutafuta kwingineko zaidi ya amri za Yesu katika Injili na Katika kuongozwa Kwa Roho Mtakatifu, tukihubiri na kufundisha hadharani na nyumba kwa nyumba. Kanisa litapandwa! Makanisa mengi yatapandwa! Kukua kwa kanisa ni wakati watu wanapolishwa na kukua na kutunzwa na kufundishwa katika kukua katika mambo yote katika Kristo.

Sura ya 2:
Kulipanda Kanisa

KANISA LINAPANDWA NYUMBANI

Katika Agano Jipya, ni wazi kuwa kanisa lilikutanika katika nymba. **1Kor.16:19** ***"Akila na Priska wanawasalimu sana katika Bwana, pamoja na kanisa lililoko ndani ya nyumba yao."***
Rum.16:3 ***"Nisalimieni Priska na Akila, watenda kazi pamoja nami katika Kristo Yesu."*** **a.4** ***"pia lisalimieni kanisa lililomo katika nyumba yao."***

Japo kanisa kule Yerusalemu liliendelea hekaluni naye Paulo aligodesha shule ya Tirano kule Efeso, kanisa la Agano Jipya kwa wingi lilikutana katika nyumba. Hili halina ubishi. Kanisa la kisasa linatakiwa kuja kufahamu na kurudia ushuhuda wa biblia na lirudie matendo ambayo mitume walifanya. Mpaka kanisa litakapo rudia matendo ya biblia – walikutana kila siku pamoja katika hekalu na nyumba kwa nyumba – hatutaushuhudia ufuvio kwa namna tunayoutamani. [hekalu laweza kuonekana kama mjengo ambao umewekwa wakfu leo, hata hivyo hekalu na shule ya Paulo kule Efeso walikutana kila siku].

Katika **Matendo 16:13-15** twasoma habari juu ya Lidia ***"ambaye moyo wake ulifunguliwa na Bwana."*** Alipobatizwa akamsihi Paulo ***"kama mmeniona kuwa mwaminifu kwa Bwana, ingieni nyumbani mwangu mkakae."*** Inaonekana kanisa lilikua katika nyumba yake, na hapo ndipo wandugu walikutanika, **a.40** ***"nao wakatoka gerezani wakaingia nyumbani mwa Lidia; na walipokwisha kuonana na ndugu, wakawafariji wakaenda zao."***

Muundo wa Biblia wa kupanda kanisa ni katika nyumba. **Mitume walihudumu nyumba kwa nyumba.** Waliumega mkate [waliishiriki meza] katika nyumba. Waliwaalika watu katika nyumba zao. Walikutana kila siku. Huduma nyingi leo hazihudumu katika nyumba kwa nyumba. Kule Myanmar ambako tumehudumu mara nyingi, serekali hairuhusu kanisa kuwa na jengo la hadhara. Ni furaha kuu kuhudumu kutoka nyumba kwa nyumba katika hilo taifa. Ndiyo, kuna sehemu ambazo ni za hadhara ambapo Shule za biblia na kanisa hukutanika na tumehudumu huko pia. Kanisa linalokuwa vema hukutana kila siku, hekaluni na nyumba kwa nyumba.

Huduma katika utano ilikuwa ya hekaluni na nyumba kwa nyumba
Matendo 2:42 ***"Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali.*** **a46** ***"Na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe."***

Matendo 20:20-21 ***"Sikujiepusha katika kuwatangazia Neno lo lote liwezalo kuwafaa bali niliwafundisha wazi wazi, na nyumba kwa nyumba, nikiwashuhudia Wayahudi na Wayunani wamtubie Mungu na kumwamwamini Bwana Wetu Yesu Kristo"***

HATUA SABA KATIKA HUDUMA INAYOFAA KATIKA KUTII TUME KUU NA KUTHIBITISHA MAKANISA YA AGANO JIPYA

Kuna hatua saba ambazo zitaweza kutusidia kuzaa matunda tunapotii mwito mkuu [tume kuu] na kuyathibitisha makanisa ya Agano Jipya.

1. Maombi
2. Uinjilisti
3. Kulisha
4. Kufundisha
5. Kujenga

6. Kupanda makanisa
7. Kujitokeza kwa kanisa la Agano Jipya

Hizi hatua ni muundo wa Maandiko Matakatifu. Muinjilisti, Dick Reuben, hufundisha kuwa tukitii muundo wa Maandiko Matakatifu, basi tutatarajia ahadi zilizomo katika Neno kutimizwa. Kwa maneno mengine tuyafanye mambo kulingana na Neno. Tazama **Yohana** anavyosema kuhusu hayo **Sura.14:12-24**, tukimpenda Yesu, tutazishika amri zake. Kisha tutaona matunda, hata ***"matendo makuu"***. Mungu alimwambia **Yoshua, 1:7**, ***"Uwe hodari tu na ushujaa, uangalie kutenda sawa sawa na sheria yote aliyokuamuru Musa …; usiiache, kwenda mkono wa kuume au wa kushoto, upate kufanikiwa sana kila uendako."*** Hizi hatua saba ni mfano wa kanisa la Agano Jipya. Tukijitolea kulitenda hili Neno tutafaulu kupanda makanisa mengi, na kuona yakikamilika.

Hatua ambayo Mungu anataka tuchukue ni **Kupanda kanisa kila mahali ulipo**. Hili laweza kumaanisha kuondoka na kwenda katika maeneo mapya; au mahali pale ulipo. Muhimu ni tubadilishe mawazo na tuwe na bidii katika utendaji kwa kufahamu yale Mungu anataka: yeye hana haja na umati wa watu! Anatuita tumfuate na tuwafanye watu kuwa wanafunzi!

KUPANDA KANISA

Tunawezaje kupanda kanisa? Ni hatuagani zaweza kuzaa matunda katika huduma? Tutawezaje kutimiza tume kuu?
Kuna hatua mbili za kupanda Kanisa: Maombi na uinjilisti.
MAOMBI: kusanyika na kuomba katika makubaliano kwa ajili ya kutimia kwa mapenzi ya Mungu;
UINJILISTI: tendo baada ya maombi.
Ukiwa mwaminifu katika kutekeleza hayo umelipanda kanisa mpya katika mda mfupi sana.

TUNAANZIA WAPI?

Kukusanyika katika Jina Lake

Tunahitaji kuwa wangapi?

Matt.18:20 ***"kwa maana walipo wawili ama watatu wanaokusanyika katika Jina Langu, Mimi niko katikati yao."*** Yesu ameahidi kuwepo wakati wawili ama watatu wanapokutana mahali pamoja katika Jina Lake na kuanza kuomba, na hili lifanyike hadi Bwana atakaporudi.

Tutakusnyika wapi katika Jina Lake?

Mahali po pote lakini nyumbani ni bora zaidi maana hapo tunaweza kufikia mahitaji ya kumega mkate, ushirika, mafundisho na maombi kwa urahisi. Watu wanatakikana kujua mahali ambapo wanaweza kupata kanisa likiomba.

Tunatakiwa kukutana lini?

Mara nyingi iwezekanavyo – kanisa la asili lilikuta kila siku.
Ebr.11:6 inaahidi kuwa atawatuza wanao mtafuta.

Tunaweza kukutana mara ngapi?

Ikiwa tunakutana kila siku, nusu saa hadi saa nzima labda ni mda mrefu. Wale wanaokutana mara kwa mara hujifunza haraka jinsi ya kuingia katika uwepo wa Bwana. Tunapokusanyika katika Jina la Yesu Kristo, uwepo wake unakaa kati kati ya watu wake. Karama za Roho zitafanya kazi kwa uhuru.Neno la maarifa, Neno la unabii, maono yanadhihirika na kutoka kwa haya tutaona mapenzi ya Mungu na mipango Yake na tutaweza kuomba na kutenda ipasavyo.

Hili ni kanisa lenye matendo. Watu wataondoka katika mkutano wa maombi kwenda kushuhudia, wakiona injili ikifanya kazi, na watarudi kwa furaha. Kutakuwa na kuzaa matunda, ambayo hujenga imani, na huleta matunda zaidi, na kuwajulisha wengine waliohudhuria ushuhuda wa nguvu na wa yale yanayotendeka kila siku.

TUNAANZA KUPANDA KANISA KATIKA MAOMBI

TUNAOMBAJE?

Kubaliana na Neno Lake

Matt.18:19 ***"Tena, nawaambia yakwamba wawili wenu watakapopatana duniani katika jambo lo lote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba yangu wa Mbinguni."*** Tunakusanyika katika jina Lake kukubaliana na mapenzi ya Mungu, yaani, kuihubiri injili kwa wale walio karibu nasi.

Omba kulingana na mapenzi Yake

Bwana anatuamuru kuihubiri injili na kuwafanya wanafunzi.

Matt.28:19 ***"Basi, enendeni, ulimwenguni kote mkawafanye mataifa kuwa wanafunzi, mkiwabatiza katika Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu."***

Marko 16:15-16 ***"Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa."***

a.20 ***"Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa."***

Luka 24:46-49 ***"Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya Tatu, na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu. Nanyi ndinyi mashahidi wa mambo haya. Na tazama nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu."***

Yohana 21:15-17 Yesu anaauru Petro ***"Kulisha wana-kondoo," "chunga kondoo wangu," "Lisha kondoo zangu."***

Omba watenda-kazi wapelekwe kuihubiri injili.

Matt.9:37-38 ***"Ndipo alipowambia wanafunzi wake, Mavuno ni mengi, lakini watendakazi ni wachache. Basi mwombeni Bwana wa Mavuno, apeleke watenda-kazi katika mavunu yake"***

Ombea nafsi za watu kuokoka. Sio mapenzi ya Mungu mmoja apotee.

2Pet.3:9 ***"Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu yeyote apotee, bali wote wafikilie toba."***

Ombea walipotea kwa majina

Yoh. 6:44 ***"hakuna mtu awezaye kuja kwangu, asipovutwa na Baba aliyenipeleka; nami nitamfufua siku ya mwisho."***

Yoh. 6:65 ***"Kwa sababu hiyo nimewaambia ya kwamba hakuna mtu awezaye kuja kwangu asipokuwa amejaaliwa na Baba Yangu."***

Zab.2:8 ***"Uniombe nami nitakupa mataifa kuwa urithi wako, na miisho ya dunia kuwa milki yako."***

Yesu akawaambia, ***"Ombeni na mtapewa; tafuteni na mtapata; bisheni na milango utafunguliwa."*** (**Matt.7:7**).

Tarajia ufunuo wa mpango

Tunapo mtii Bwana, Atafunua / atauweka wazi mpango kwa ajili yetu. Yeye ndiye aliyesema, ***"Nitawafanya wavuvi wa watu,"*** (**Matt.4:19**). Ameahidi kutuonyesha yale yatakao kuja, (**Yoh. 16:13**).

KWA HIVYO TUNAANZIA

- Palipo na wawili au watatu waliokusanyika pamoja – katika nyumba
- Wakimtambua Mungu miongoni mwao
- Biblia ikiwa wazi kwa kuombea mapenzi ya Mungu yafanyike: ***"Ufalme wako uje."***
- Omba kwa bidii kwa ajili ya waliopotea
- Maombi ya vita – kumnyima shetani nafasi ya kumzuia yeyote katika utumwa kwa kutambua nguvu za Mungu na kutambua mapenzi ya Mungu kuwa wote waokoke (**1 Tim.2:1-4**)
- Kuombea watu kwa majina
- Kuombea wilaya, makundi ya watu, mataifa
- Kumuomba Bwana wa mavuno kwa ajili ya watenda-kazi
- Tukitarajia Mungu kufanya yale alisema atafanya
- Shukuru kwa kile atafanya na yale anatenda

Kanisa la nyumbani linapokutana na kuendelea katika maombi, Mungu anajibu maombi. Mawasiliano yanafanywa kwa njia ya Mungu.

Baada ya maombi ni matendo! Maombi ya kila wakati yenye msingi wake kwa Neno la Mungu, huleta matunda mengi, yaani, nafsi nyingi zinaokoka, na wengine wanatiwa nguvu kumzalia Bwana matunda.

KUOMBA KATIKA MAONO

HabakukI 2:1-3 yatupatia mfano wa yale tunatakiwa kufanya katika maombi.

a.1 ***"Mimi nitasimama katika zamu yangu, nitajiweka juu ya mnara, nitaangalia ili nione atakaloniambia, na jinsi nitakavyojibu katika habari ya kulalamika kwangu."***

Tukeshe katika maombi, Bwana anaweza kutuonyesha maono. Tumngojee Bwana anene, ngojea jibu Lake.

a.2 ***"Bwana akanijibu akaniambia, andika njozi ukaifanye iwe wazi sana katika vibao, ili aisomaye…."***

Tuandike chini maono ambayo Bwana anatuonyesha – mapenzi ya Mungu.

a.3 ***"maana njozi hii bado ni ya wakati ulioamriwa, inafanya haraka ili kuufikilia mwisho wake, wala haitasema uongo, ijapokawia, ingojee, kwa kuwa haina budi kuja, haitakawia."***

Tuyangojee maono yetu kutimia – tuombe katika mapenzi ya Mungu – tuombee maono hayo yatimie. Haitakosa kutimia kwa sababu ni ya Mungu.

KUENDELEA KUJENGA JUU YA MSINGI WA MAOMBI

Tunaweka msingi wa yale yote tunayofanya katika maombi na tujenge juu ya huo msingi jinsi Mungu anavyoelekeze na kututia nguvu. Kanisa hilo linalokutana kwa Nyumba, waliokusanyika kwa maombi, linafanyika mwili wa kuwatuma. Watenda-kazi wanaenda shambani wakiwa na nguvu kutoka katika kituo chao ambapo wanakutana na Bwana katika kanisa la nyumba. Maombi huendelea mpaka kazi imalizike. Bwana atakuja wakati ambapo uinjilisti wetu binafsi utakapo kamilika

UINJILISTI

Hatua ya nguvu inayofuata. Kanisa tayari limepandwa, na linaendelea na wawili au watatu kama washirika. Baada ya Maombi huja uinjilisti. Mungu anaanza kuokoa wengine. Muinjilisti anawakusanya waliookoka, lakini kila mwanafunzi wa Yesu anatakiwa kuwa shahidi, baada ya kupokea nguvu za Roho Mtakatifu, (**Matendo 1:8; Luka.24:48-49**).

KUENDA NJE NA UJUMBE

Uinjilisti unamaanisha ***'kuenda nje na ujumbe'***. Twende na ujumbe wa wokovu katika Jina la Yesu Kristo. Wakati Filipo alipoenda Samaria, (**Matendo 8:12**) alihubiri Jina la Yesu na ufalme wa Mungu. Mji wote ulisikia na kuona matendo makuu ya Mungu yaliyofanywa kwa mikono yake. Baada ya maombi Mungu ataelekeza kwa sababu mmekuja pamoja katika maombi ya makubaliano kuhusu mapenzi ya Mungu. Baada ya kufunga na kufungua unaenda kuchukua sehemu uliyokuwa ukiteka katika maombi.

Marko 16:15 ***"Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri injili kwa kila kiumbe."*** Hii ni amri aliyotoa Yesu, ni lazima tutii. Amesema ***"ukinipenda mimi, utazishika amri zangu."*** Ni lazima tutii Tume Kuu ili twende ulimwenguni kote kuihubiri Injili.

IMANI PAMOJA NA UBATIZO NI WOKOVU

v.16 ***"Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa."*** Kutakuwa na wale ambao hawataamini. Lakini amri ni kwamba twende tukaihubiri Injili. Neno ni Enendeni. Milango ya kuzimu haitaweza kushinda kanisa ya Mungu ambalo linapandwa na kukuswa.

JINSI LINAVYOZALIWA

'Jinsi ya kuzaliwa' imewekwa wazi katika Agano Jipya ambalo hatuna budi ila kutii. Katika **Matt.28:19** na **Marko 16:16** Yesu wazi wazi anaelezea kuwa ubatizo wa maji mengi ni jambo mojawapo muhimu katika safari ya wokovu. Wale wanaookoka wanatakiwa kubatizwa katika maji mengi siku hiyo ambayo wamekubali kuamini (**Matendo 2:38-41, 10:44-48, 19:1-6**). Pia, wanatakiwa wapokee kipawa cha Roho Mtakatifu (**Matendo 2:38, 8:14-17, 10:44, 19:6**). Ni jambo la muhimu sasa kuanza kujiuliza jinsi ambavyo tumekuwa *'tukiokoa nafsi'* kwa kuwaongoza tu *'katika ombi la toba'* bila kuwaamuru wabatizwe katika maji mengi na kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Hebu fikiria jinsi gani wanaookoka watakavyokuwa hodari mara tu wanapozaliwa upya: toba, imani na mabatizo.

ISHARA ZIKIFUATA

a.17-18 ***"Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya."*** Hizi ni ishara ambazo tunatarajia zitawafuata wote waaminio. Hizi ishara zinapatikana katika nyumba, katika Hekalu, katika darasa ya Tirano, na katika barabara kama ilivyo nukuliwa katika kitabu cha Matendo ya Mitume.

a.19 ***"Basi, Bwana Yesu baada ya kusema nao, akachukuliwa juu mbinguni, akaketi mkono wa kuume wa Mungu."*** Yesu alipokelewa mbinguni nao mitume, ***"wakatoka, wakahubiri kote-kote, Bwana akitenda kazi pamoja nao, na kulithibitisha lile Neno kwa ishara zilizofuatana nao."*** ***a*.20.** Bwana wakati wote atalithibitisha Neno Lake na ishara zikifuata.

UPAKO KWA AJILI YA UINJILISTI

Twastahili kujua kuwa kuna upako tofauti kati ya kanisa linalokutana kanisani na ule wa kwenda nje katika barabara. Tunahitaji upako wa uinjilisti tunapoenda huko nje, na sio upako tulionao wakati tunapoabudu mahali Patakatifu. Hata hivyo, katika mkutano wa nyumba wakati kuna watu ambao hawajaokoka, upako wa BWANA utawezesha hilo kanisa la nyumba kuwa mahali pa kupanda mbegu kwa ajili wale ambao hawajaokoka kufanya hivyo.

KUTOKA KUWA WATOTO HADI KUKAMILIKA

Mtume Yohana anaandikia makundi matatu katika kanisa katika **1 Yoh.2:12-14**. Anawaandikia ***"watoto wadogo"***, na ***"vijana"***, na akina ***"baba"***. Hivi vizazi vitatu pia vinahuzisha kanisa; kanisa la utoto, kanisa ambalo linakua katika ujana na kanisa ambalo limekomaa, kamilifu ambalo

limekua ndani ya Kristo katika mambo yote, ambaye ndiye Kichwa. (**Efe.4:15**). Mafunzo yake Yohana yanatusaidia kuelewa kupanda, kukusa na kukomaza kanisa. Watoto wadogo ni wale ambao wameokoka na wanahitaji maziwa ya Neno ili wakuwe kwalo. Vijana wanawakilisha wale ambao wamefundishwa Neno na wamemshinda Yule muovu. Akina baba ni wale wakamilifu ambao wamefikia ufahamu wa juu katika uhusiano na Baba. Vijana wanaweza kuwaongoza wengine kwa Kristo na kufundisha misingi kwa wale Wakristo wachanga. Akina baba ni kipawa cha huduma baada ya kupaa [mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji na waalimu] ambao hulileta kanisa katika ukamilifu.

Kanisa changa ni wawili au watatu wanaokutanika, kuombea waliopotea. Hili ni kanisa ambalo **linafaulu katika kuwaleta wengi kwa Kristo**.

Kanisa la ujanani ni kanisa linalokutana katika nyumba **likihimiza na kufunza wakristo wote wachanga**.

Kanisa lililokomaa / kamilifu ni kanisa la kiutume ambamo **karama zote na huduma zinafanya kazi** wazi wazi na kutoka nyumba kwa nyumba, kulileta kanisa lote kwa ukamilifu.

Sura ya 3:
Kukusa Kanisa

KUKUA NI NINI?
Neno 'kukua' halijatumiwa sana katika Biblia kwa njia ya kusema 'watu zaidi'. Mara nyingi limetumiwa kuonyesha hali ya kukua kutoka kuwa Wakristo wachanga hadi kuwa Wakristo waliokomaa. Kukua kwa kanisa ni wakati kanisa lote na kila mtu binafsi amekomaa. Kupanda kanisa tunawakamata wale wachanga na kuanza kuwasaidia kukua, awe muhudumu, mtume, nabii, muinjilisti, mchungaji au mwalimu au mtenda miujiza au mtu wa karama yo yote ambayo Mungu amepeana. Kukua kuzuri ni kule tunaona mkristo mchanga anakua na kufanyika mhudumu mzuri katika mwili.

KUCHUKUWA HATUA ZA HUDUMA YENYE MAZAO
Kuna hatua saba katika huduma hii kwa ajili ya kutimiza Tume Kuu na kuweza kusitawisha makanisa ya Agano Jipya. Katika kipndi kilichomalizika tulitazama **kazi ya msingi wa Maombi** katika kutii Tume Kuu katika kusitawisha kanisa ndani nyumba. Baada ya maombi tunaondoka na kufanya uinjilisti. Bwana anayajibu maombi kwa kuwaleta watu wengi kuokoka. Maombi hufanya **kutimia kwa maono ya kuwafikia waliopotea**. **Tunapanda kanisa katika maombi.** **Maombi yatatuongoza katika kufanya kazi ya uinjilisti** – nafsi nyingi zinaletwa kanisani na kuanza kutunzwa.

Kanisa **linapandwa katika maombi na uinjilisti**;
Kanisa **linakua kwa kutunza na kufundisha**.

KUTUNZA
Hatua ya tatu katika kutimiza huduma yenye manufaa ni kutunza wale walio wachanga wa imani. **Kutunza ni kulea Mkristo mchanga.** Mtume Yohana aliwaita Wakristo wachanga kama watoto wadogo, na katika **1Yoh.2:12-14**, ananukuu mambo mawili muhimu juu yao:
1. **Wamesamehewa dhambi** kwa ajili ya Jina Lake na
2. **kwa sababu mmemjua Baba**.

Wakati mtu anapookoka (**Yoh.3:3-6**) anafanyika kiungo katika jamii ya Mungu, ***"Ambao hawakuzaliwa kwa damu, wala kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mwanadamu, bali ya Mungu,"*** **Yoh.1:13**. Roho Mtakatifu anapoingia ndani ya roho ya mtu anampa huyo mtu ***"Roho wakufanyika kuwa Mwana, ambapo twalia, Aba Baba,"*** **Rum.8:15**.
"Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, yakuwa sisi tu watoto wa Mungu." **Rum.8:16**.

TUNATUNZA AJE WATOTO KATIKA KRISTO?
MAZIWA YA NENO
Kwa kuwalisha: Yesu alimuamuru Petro ***"lisha wana-kondoo"*** (**Yoh.21:15**) na ***"lisha kondoo"*** (**a.17**). watoto wanahitaji maziwa, kwa hivyo tunawalisha **maziwa ya Neno la Mungu**. Kondoo wanahitaji **chakula kigumu**.
1 Pet.2:2 ***"kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu."*** Hii ni habari njema ya wokovu: kama mtume Yohana alivyosema, kujua dhambi zako zimesamehewa.

KANUNI ZA MSINGI
Katika **Ebr.5:12**, mtume anasema ***"mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu"***, yaani, ***"misingi"***, (**Ebr.6:1-2**) ni maziwa ya Neno la Mungu. Anawahimiza Waebrania kukaza mwendo

ili waufikilie utimilifu na wasiweke tena misingi sita. Kwa hivyo ni wazi katika **Ebr.5:12 – 6:3** kwamba **kufundisha kanuni za kwanza ni kulisha maziwa ya Neno la Mungu.** **Chakula kigumu ni Neno la haki** (**Ebr.5:13**) na chakula kigumu ni cha waliokamilika.

KUWEZESHWA KUFUNZA
"kwa maana iwapasapo kuwa walimu" (**Ebr.5:12**)
Hawa Wakristo ambao mwandishi kwa Waebrania anaandikia wangekuwa wamekua, lakini mda mwingi umepita na wangali watoto; bado wanahitaji kunyweshwa maziwa. Maziwa ni ya watoto. Mtume anataka walishwe chakula kigumu. Thibitishao kuwa hawajakua ni kwamba hawawezi kuwafundisha wengine misingi ya imani. Kila mmoja anatakiwa afundishwe kanuni za kwanza za Neno la Mungu. Mara tu unapopewa maziwa, unaanza kukua, na unawezeshwa kufundisha wengine na kutambua mafundisho ya uongo.

KUKUA
Lengo la Mungu kwetu ni tukue katika Bwana ili tuweze kuwafundusha wengine. **2Tim.2:2** ***"mambo uliyoyasikia kutoka kwangu, uwakabidhi watu walio waaminifu ambao watawafundisha wengine pia."***
Ebr.5:13 inaelezea kuhusu Yule ***"asiyekuwa na ujuzi katika Neno la haki huyu bado ni mtoto.*** Neno la haki ni chakula kigumu. Kuweza kufahamu na kuhubiri na kufundisha na kuishi kwa Neno la haki ni kuwa Mkristo aliye komaa.

TUSIWE TENA WATOTO WACHANGA
Eph.4:14 ***"tukitupwa huku na huku na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu;"***; tusiwe watu wa kufuata mtu Fulani na mafunzo yake, bali tuwe **wanafunzi wa Neno sisi Wenyewe**. Kuyachunguza maandiko sisi wenyewe kujua kama ni kweli yale unayoyasikia au la. Tazama mfano wa Waberea katika **Matendo 17:10-12**.
"Chakula kigumu ni cha watu wazima" (**Ebr.5:14**). Wanaoweza kupambanua kati ya Mungu na shetani ni wale walio na Roho Mtakatifu na zaidi hao ambao wamekomaa katika Neno la Mungu.

TUTAWEZAJE KUMTUNZA MKRISTO MCHANGA?
WOKOVU, UPONYAJI, UREJESHO
Tunawalisha Neno la Mungu. Wakristo wachanga wanahitaji kufundishwa na kufanywa kuwa wanafunzi. Ni mafundisho ya Neno la Mungu ndiyo hufunza, hurekebisha, huonya na kuadhibisha katika haki. (**2 Tim.3:16**). Wanahitaji kufundishwa Neno kuhusu **wokovu**, Neno kuhusu **uponyaji**, Neno kuhusu **urejesho**.

KUWEKWA MSINGI KATIKA IMANI
Ebr.6:1-2, ya orodhesha misingi sita, na ina sema kuwa tusipo kuwa tumewekwa vizuri katika hiyo misingi hatutaweza kukaza mwendo na kuufikilia **utimilifu/ukomavu**. Misingi hi ni: **Kuzitubia kazi zisizo na uhai**, **kuwa na imani kwa Mungu**, **mafundisho ya mabatizo**, **kuwekea mikono**, **kufufuliwa wafu**, na ya **hukumu ya milele**. Kutunza kunamaanisha kuwaongoza Wakristo wachanga katika misingi hii na kuhakikisha kuwa kila moja yake imewekwa vizuri. Wakati ambapo Mkristo mchanga amewekwa kwenye msingi mzuri wa imani katika Neno la Mungu watakua. Hii itaweka msingi uliomzuri kwa kanisa kuufikia utimilifu.

KUDUMU KATIKA MATENDO YA KWANZA
Siku ya Pentekoste, Roho Mtakatifu alimwagwa, na watu 3000 wakapata kuokoka. Hawa Wakristo wachanga waliendelea katika mambo manne: **fundisho la mitume, ushirika, kumega mkate na kusali**, (**Matendo 2:41-42**). Hapa tunapata kile ambacho tunastahili kuwalisha tunapowachunga wakristo wachanga, ili wakue na wathibitishwe katika imani. Katika kanisa la biblia la nyumba, haya mambo manne yalitendeka. Katika kitabu cha Matendo ya Mitume,

mitume walifundisha katika nyumba na pia wazi. Wale ambao Yesu alifundisha walikuja na kushiriki katika nyumba. Ishara na maajabu ikitendeka katika mikutano ya nyumba. Walimega mkate nyumba kwa nyumba. Tazama **Kumbu 6:4-8** kanisa la nyumba kulingana na Sheria ya Musa.

Kila kitu ambacho ni cha muhimu katika maisha ya Mkristo kinapokelewa katika njia ya ubatizo katika Mwili, (**1 Kor.12:13**). Mkristo mchanga anakua katika mambo yote katika Kristo kwa sababu ujuzi wa kuokoka na kubatizwa kujiunga na kanisa na kubatizwa kwa Roho katika mwili. Kanisa ambalo linaendelea kulingana na fundisho la mitume na matendo ya ya kwanza ya kanisa ambayo yanawezesha ujuzi wa maandiko kila siku wa mafundisho, ushirika, kuumega mkate na maombi / kusali.

KUWA MWANAFUNZI

Waaminio wote wanatakiwa wafanywe kuwa wanafunzi. Yesu alisema katika **Matt.28:19** kuwa ***'tuwafanye wanafunzi***, kwa kuwafundisha kuyashika yote ambayo alikuwa ameamuru.
Lengo la kuwafanya wanafunzi ni:

1. **Kumuwezesha kila Mkristo mchanga kufundishwa Neno la Mungu**, sio mtu au kiongozi mkuu bali Neno la Mungu.
2. **Kwa kumfundisha kila aaminiye kanuni za Neno la Mungu,** ili wakaweze kukua kwazo.
3. **Kumfundisha kila mwanafunzi kujisomea Biblia**.
4. **Kumfundisha mwanafunzi jinsi ya kupokea Neno la*'rhema'* kutoka kwa Mungu**, (**Rum.10:17**).
5. **Kumpatia mwanafunzi mazoezi ya msingi ya kusoma Biblia, kujifunza, maombi na kushuhudia.**

KUWAFANYA WANAFUNZI

'Mwanafunzi' ni jina la kilatini sawa na *'nidhamu'*, yote yakitoka kwa jina la Kilatini linalomaanisha kunena au kufunza katika hali ya kuelekeza. Kwa hivyo kuwafanya wanafunzi ni huduma ya kufundisha. Inatimiza sehemu moja ya tume, kumfundisha Mkristo mchanga Neno la Mungu, (**Matt.28:20**). Kila Mkristo mchanga anatarajiwa kuwa amebatizwa kulingana na **Matendo 2:38,** amepokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Hiyo ni kazi ya uinjilisti. Basi kila aaminiye anatakikana atunzwe katika imani kwa njia ya kupokea maziwa ya Neno. Basi, sasa aaminiye yuko tayari kufanyika mwanafunzi, mufuasi wake Bwana Yesu Kristo kwa moyo wake wote, anayedumu katika kupokea amri Zake kupitia kwa Neno la Mungu.

MPANGO WA ASILI WA KUWA MWANAFUNZI

1. Dumu katika kujifunza Neno kila siku, Sura 3 – 5
2. Kunakili, kuandika chini kila sura ambayo imesomwa kila siku, na kutamatisha yale ambayo umesoma.
3. Omba Bwana kujua anasema nini katika sura hiyo uliyosoma; umuruhusu anene kutoka kwa Neno Lake. Andika chini kile Bwana ananena.
4. Jifunze kukariri aya tatu za Maandiko Matakatifu kila juma.
5. Shiriki imani yako na watu 2 kila juma.
6. Waombee waliopotea kwa majina. Nakili majina yao na majibu ya Mungu.
7. Kusanyika katika kikundi kidogo kila juma kwa saa moja pamoja na wengine ambao pia wanafunzwa Neno, na kiongozi. Hiki ni kikundi kinachowajibika, kujibu na kushiriki kile ambacho Mungu ameonyesha na kuuliza maswali.

LENGO/KUSUDI

Lengo na kusudi la kufundisha wanafunzi ni kupanda makanisa ambayo yataweza kushuhudia nguvu za Mungu. Kunahitajika kuwa na kanisa ambalo linahusika katika kufikia waliopotea,

kulingana na njia ya biblia ambalo linadhihirisha nguvu za Mungu miongoni mwake ili kila nafsi iguzwe na ifikiwe na injili.

Kituo cha kanisa ni nini?
Jamii au kikundi kidogo ambacho kinakutana pamoja na Yesu (**Matt.18:18-20**) na kutafuta kuokolewa kwa waliopotea. Kanisa linakua wakati watu wanapookoka na kujiunga na jumuia ya walioamini, wala sio watu kuhama kutoka kwa shirika zingine.

Ni nini kinacho jumuisha kanisa la Agano Jipya?
Mfano rahisi ni **Matendo 2:42-47**. Wakristo wachanga pamoja na mitume na wengine ambao walikuwa tayari ni Wakristo walidumu katika mambo manne;

- Kushiriki Neno la Mungu [fundisho la Mitume]
- Ushirika
- Kumega mkate [meza]
- Maombi / kusali

Wali yafanya haya kila siku nyumba kwa nyumba. Pia kulikuwa na huduma wazi ya kuhubiri injili, na Paulo alifundisha katika shule wakati huo.

Kanisa linaanza na watu wawili ama watatu wanaodumu katika kushiriki Neno la Mungu, wanaomba, wanamega mkate na kuingia katika uhusiano wa dhati. Katika **Matendo 2:43**, ***"wakaingiwa na hofu"***, na ***"ajabu nyingi na ishara…"***. Amini Mungu kwa ajili ya maajabu na ishara; Ishara za uwepo Wake miongoni mwao. Bwana anatumia ishara na maajabu kuwavutia watu kuja kusikia Injili. **a.44-45** kiwango cha ushirika wa matendo (ushirika) unaonyeshwa. Kanisa linatakiwa kudumu katika mambo yaya haya kila siku, (**a46**). Matokeo ni watu wa sifa, ambao wamewekwa huru katika Bwana na makusudi Yake, na anaongeza wale wanaookoka kila siku, (**a47**).

Kanisa linakua kwa njia ya kuwafikia waliopotea, kutunza na kufanya wanafunzi.
Kwa kumalizia, kanisa lina huduma mbili muhimu katika kutimiza Tume Kuu:
UINJILISTI na MAFUNDISHO.

Kuwafanya wanafunzi, tunahitaji kuhubiri injili; wanao amini na kubatizwa wataokoka na watapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kisha wataweza kufundishwa yote ambayo Yesu aliwaamuru na kuyashika. Kufanya wanafunzi ni timizo la Tume Kuu. Baada ya kufanya wanafunzi – misingi imewekwa vizuri – basi utimilifu wa kanisa utafuata haraka. Bwana atarudi na kutuingiza katika kizazi cha milenia ya saba.

Sura ya 4:
Kulikamilisha Kanisa

Lengo la kufanya wanafunzi ni kufundisha na kukamilisha wanaume kwa wanawake na kuwaingiza katika huduma inayofaa.

Kila kanisa linatakiwa kuwa:

chuo cha huduma ya mafundisho,
nyumba ya maombi kwa mataifa yote,
mahali ambapo waaminio wachanga wanatunzwa katika imani,
mahali ambapo waaminio wanafunzwa Neno la Mungu.

Lengo ni waaminio wachanga kuwa wahusika wazuri wa kanisa. Mungu mwenyewe huweka watu katika Mwili (**1Kor.12:18**). Yesu alitutuma tuwafanye wanafunzi!

Yesu alisema, ***"Enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe"*****!**
Yesu alisema, ***"Lisha wana-kondoo wangu"*****!** hii ni kutunza wakristo wachanga.
Yesu alisema, ***"Lisha kondoo zangu"*****!** huduma ya kufundisha.

"Kufanya kazi ya huduma" ni kufundisha na kukamilisha wanafunzi ili wawe wahusika katika Mwili wa Kristo. Mungu ameweka kanisani, ***"kwanza mitume, pili manabii, tatu waalimu, halafu miujiza, karama za kuponya, masaidiano, maongozi, na aina za lugha"***, **1Kor.12:28**.

Hatua ya tano ya huduma ya manufaa ni: **kufunza na kukamilisha watakatifu.**
Kanisa linakamilishwa kwa **kufunza na kukamilisha** wanafunzi.

KUKOMAA KWA KANISA

Kanisa linakomaa likielekea katika utimilifu kwa sababu watakatifu[viungo vya mwili] wanakamilishwa katika kazi ya huduma ambayo Mungu alitangulia kuandaa kwa ajili yao. (**Efe.2:10**), na wanajengwa na kukua katika ***"maarifa ya Mwana wa Mungu"*** (**Efe.4:13**).
Efe 4:7-16 inatupatia picha ya kanisa ambalo limekomaa.
aya 7-12: kila mmoja amepokea neema kwa njia ya vipawa vya huduma ambavyo Kristo amepeana.
aya13-16: kuelekea katika utimilifu, umoja wa imani, kumfahamu Mwana wa Mungu hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo; ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, nakuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu; tushike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote Kristo; mwili wote ukijijenga katika upendo.

KILA MUHUSIKA AWE MUHUDUMU

Hakuna mgawanyiko kati ya makasisi na kusanyiko katika kanisa la Kristo. Kipawa cha uongozi wa huduma cha mitume, nabii, muinjilisti, mchungaji na mwalimu kimetolewa kwa ajili ya kujenga na kukamilisha watakatifu, viungo vya mwili, kuwaleta katika kazi ya huduma ambayo Mungu amewaneemisha na kuwaitia.

Lengo la huduma ni kufundisha na kuwakamilisha wahudumu wengine wengi. Kila mshiriki wa kanisa la Kristo anatakiwa kufunzwa, atiwe mafuta na atumwe katika kutenda kazi. Sisi sote ni makuhani na wafalme; Kuhani wetu Mkuu ni Bwana Yesu Kristo. Hata japo watu wengi wanatoa huduma ya maneno matupu kwa misingi ya imani yao, ni wachache tu ndio hutekeleza. Bado tuna migawanyiko mingi katika kanisa juu ya mwito wa huduma na viwango vya upako na ukuhani.

KAZI NI MARA MBILI
Kwanza **kuwaleta watenda kazi katika mavuno – kufunza na kukamilisha, kutuma na kutawaza.**
Pili, **kufanya uinjilisti – kupanda makanisa mengi.**

KUFUNZA

Wakati mkristo mchanga anapokuwa amefunzwa vizuri [misingi yote imewekwa vizuri, **Ebr.6:1-2**] na kufundishwa [Neno kwa ufasaha, **Matt.28:20**], kunakuwa **na wakati wa kufunza na kuwaleta katika ukamilifu**.
Mkristo anaachishwa maziwa (**Ebr.5:12, 1 Pet.2:2**) anajulishwa kwa viakula vigumu, (**Ebr.5:12-14**), hekima iliyofichwa (**1Kor.2:6-16**), kufundishwa katika njia za haki.

Kiwango cha kwanza cha mafunzo ni kila mmoja ***"afunze kanuni za kwanza za Mungu"*** **Ebr.5:12**. Na kutoka hapa ataweza kuelewa ***"hekima iliyofichika"*** kuhusiana na makusudi ya Mungu (**Efe.3:8-11**); wakisha funzwa kuitafsiri torati, manabii na maandiko (**Lu.24:44-45**);
Kukua katika kuufahamu unabii, kufahamu Hema ya Musa (**Ebr.9:1-5**), Sikukuu za Israeli, mfano wa milkizedeki na mambo mengine mengi yanayofundishwa katika kitabu cha **Waebrania**.

Paulo alimwambia Timotheo ***"Na mambo ambayo umeyasikia kutoka kwangu mbele ya mashshidi wengi, wakabidhi watu waliowaaminifu watakowafundisha wengine."*** **2 Tim.2:2**.
Paulo alipokea ufunuo wake kutoka kwa Kristo. Paulo alimfunza Timotheo, miongoni mwa wengine. Timotheo anatakiwa awafundishe watu waaminifu yale aliyojifunza. Hawa nao wataweza kuwafunza wengine; waanzishe kanisa la nyumba; wafunze misingi n.k.

Kufundishwa ni kuelemisha hadi anaye elimishwa ahitimu
Katika Neno na kuweza kuwafunza wengine!

KUKAMILISHA

Kukamilisha ni **kufunza katika huduma**; **kufahamu na kufanya huduma katika Roho**, (**2 Kor.3:2-6**) na **kuenenda katika karama za Roho Mtakatifu** (**1 Kor.12:4-11**). Inajumuisha kutembea katika vipawa vya Neema vya **Warumi 12:4-8** na kutambua vipawa hivi katika maisha ya wateule, **kuwatia moyo kuendelea katika hivyo vipawa** ambavyo wamepewa. Kunahitajika kuwa na **mafunzo na utekelezaji wa huduma ya Efe.4:7-12**, ili wanaofunzwa waweze kutenda kazi katika kipawa cha Kristo aliye paa. Sio watu wote walioitwa katika karama za Kristo aliyepaa, lakini ni lazima wafunzwe kuhusiana na hizo karama na wanahitaji kuona karama hizi zikitenda kazi wanapoipokea neema ya kukua katika ukamilifu.

Kukamilishwa ni kuwezeshwa kujua na kuelewa na kuenenda katika njia za Mungu
Katika Roho; kuhudumu katika nguvu za Roho Mtakatifu.

Kufunza na kukamilisha kunahusisha **kufunza, kutenda na kuwa na ujuzi**. Kunahusisha kukamilisha mafunzo Fulani, warsha zingine, kuwa katika vikundi vya huduma, na kujifunza jinsi ya kufanya kazi ya huduma. **Efe.4:12**.

HUDUMA KATIKA ROHO
Ni nini kinachohudumiwa?
Kuwekea mikono, **vipawa vya Roho** vinahudumiwa; wengine wanaweza kuachiliwa katika vipawa vya Roho Mtakatifu; wengine wanaweza kupokea kipawa Fulani ambacho Mungu anawapa kama kuponya wagonjwa. Huyu anaweza kufanya kazi katika huduma ya uponyaji katika kanisa.

Upako wa Roho Mtakatifu unatumiwa; upako unaachiliwa kwao kwa kuwekea mikono.Wakati mwingine upako unakuwa mkuu sana mahali palipo na uwepo wa Mungu ambapo upako unaoshuka ni mkuu sana kiasi kuwa watu wanapokea bila kuwekewa mikono. Kila mtu pale anaadhirika.

Nguvu za Mungu zinathihirika katika huduma. Yesu alitoka jangwani ***"katika nguvu za Roho"*** (**Lu.4:14**) kuanza kazi yake ya wazi / hadhara. Nguvu za Mungu zinashuka wakati ambapo watakatifu wanapotambua ushindi katika Kristo juu ya shetani. Mitume wanaofundisha wanatakiwa kujua nguvu na mahitaji ya kukamilisha katika kujua uwezo wa Roho Mtakatifu wa Mungu kuweza kuwapa wengine pia uwezo huo.

KUTUMA

Kunafika wakati ambapo mtu yuko tayari kufanya kazi. Mtu anaweza kuwekewa mikono wakati huu na atengwe kwa ajili ya huduma maalum; ama wanaweza kuanza kuhudumu na muda si muda, huduma hiyo inathihirika. Ni jambo la ajabu unapowekewa mikono baada ya kipindi cha mafunzo na kukamilishwa na kisha kutumwa kwenda kuhudumu. Tunamuona Bwana akifanya haya pamoja na mitume katika **Marko 6:7-13**, wale sabini **Luka 10:1-12**.

KUTAWAZWA

Kutawazwa ni kupewa mamlaka ya kuhudumu. Kutawazwa kunatendeka kama thihirisho la wazi kuhusu huduma ambayo tayari inaonekana: pale ambapo mtu anathihirisha karama ama uwezo ambao unadhuru utekelezaji wa huduma; pale ambapo mtu anatambua mwito wa Mungu juu yake kuwa muhudumu; na maisha yao yanaonyesha kuwa wanaweza kutawazwa (**1 Tim.3:1-7, Tit.1:5-9**).

Huduma ambayo tunawatawaza watu ni **Efe.4:7-12**. Wakati mwingi watu hupewa cheo cha Mchungaji, na hii inafaa wakati anapokuwa anahudumu kama mzee anayetunza na kulinda kundi la Mungu, tunawatawaza katika huduma ili wasije wakapungukiwa kwa lo lote katika huduma ya Efeso. Hii inamaanisha kuwa mtu anaweza kuhudumu kama mtume, nabii, muinjilisti, mchungaji na mwalimu pamoja na kuwa mchungaji.

<u>Kutawazwa kulingana na biblia ni</u>:

1Tim.4:14 "*Usiwache kutumia karama ile iliyomo ndani yako, uliyopewa kwa unabii na kwa kuwekewa mikono ya wazee.".*
2Tim.1:6 *"kwa sababu hiyo nakukumbusha, uichochee karama ya Mungu iliyo ndani yako kwa kuwekewa mikono yangu."*
Matendo 6:6 *"ambao wakawaweka mbele ya mitume, na walipokwisha kuomba, wakaweka mikono yao juu yao."*
Matendo 13:2-3 *"Basi hawa walipokuwa wakimfanyia Bwana ibada na kufunga, Roho Mtakatifu akasema, Nitengeeni Barnaba na Sauli kwa kazi ile niliyowaitia. Ndipo wakiisha kuomba na kufunga, wakaweka mikono yao juu yao, wakawaacha waende zao."*

Kutoka. 28:41 *"Nawe mvike huyo nduguyo Haruni na wanawe nao mavazi hayo; nawe watie mafuta, na kuwaweka kwa kazi takatifu, na kuwatakasa, ili wapate kunitumikia mimi katika kazi ya ukuhani."* Musa alipewa maelezo ya kuvisha mavazi la ukuhani Haruni na wanawe.

MUNGU ANATIA MAFUTA, WAZEE WANATAWAZA, MAISHA YA MTU YANATAKASWA.
Katika tafsiri ya New Americian Standard Bible, **aya 41b** inasema, ***"Uta <u>tia mafuta</u> juu yao na <u>uwatawaze</u> na <u>uwatakase</u>, ili wanitumikie kama makuhani."***

Kuelewa mstari huu: Mungu anapaka [anamwagia mafuta] (**2 Kor.1:21**)
Wazee wanatawaza kwa kuwekea mikono(**1Tim4:14**)
Mtu anayetawazwa anakuwa ametengwa kwa ajili ya Bwana.
Neno *'Tawaza'* linajumulisha majina mawili ya kibrania, ambayo yanamaanisha *"kuujaza mkono".* Kutawaza basi ni kutuma karama na huduma.

KUFUNDISHA KATIKA KAZI
Tunajua kuwa kuandaa mtu kwa ajili ya kutawazwa ni kufundisha katika kazi ambayo inalingana na mfano wa Biblia. Mtu kwanza anakuwa mwanafunzi ambaye anajiunga ama ana ambatana na mhudumu ambaya tayari ametawazwa katika hali ya kufundisha, kuhubiri na huduma inatekelezwa. Yule ambaye anafundishwa anajifunza kwa kuangalia, na maelezo na kutenda.

KUFANYA KAZI YA UINJILISTI
KUPANDA MAKANISA MAPYA

Hatua ya sita katika kuendeleza huduma inayofaa katika kutimiza Tume Kuu ni
Kupanda makanisa mapya.

Kila mwanafunzi wake Yesu anatakiwa awe shahidi, baada ya kupokea Roho Mtakatifu (**Matendo 1:8, Luka.24:48-49**). Kutoa ushuhuda unahusisha kuthihirishwa Nguvu zake ambao unaleta watu kwa Kristo. Katika Maandiko Matakatifu, watu waliongezeka kwa kanisa:
Kwa kuitikia Neno lililohubiriwa, **Matendo 2:37**
Kwa kuthihirika kwa Nguvu za Mungu, **Matendos 8:5-8, 12; 1 Kor.2:4-5**
Kwa kuvutiwa na matendo yaliyokuwa ya kwanza, **Matendo 2:42-47**

Uinjilisti ni matendo ambayo yanatokana na maombi: maombi ya uinjilisti. Njia ya uinjilisti ni maombi. Lengo ni mioyo iokolewe. Mpango ni kupanda kanisa, ili kwamba waliopotea waongezeke kuja kanisani. Kunahitajika kuwepo kwa kanisa linalowatafuta waliopotea, linalo shuhudia **miongoni mwa kila watu na makundi**.

KUPANDA KANISA:
Wale ambao wamefundishwa na kukamilishwa wanatumwa. Kanisa jipya linajitokeza kwa sababu nafsi mpya zina okoka. Zinaendelea kuongezeka kwa sabau watu wanaokoka kila siku. Kanisa la Agano Jipya halikukosa kuhubiri na kufundisha Neno la Mungu, wakitangaza Injili ya Bwana wetu Yesu Kristo kila siku, hadharani na nyumba kwa nyumba. **Matendo 5:42**

KILA MAHALI
Tulianza muongozo wa hiki kitabu na himizo kubwa la kurudia Maandiko Matakatifu kwa mamlaka na kutuongoza kuelewa kanisa, na kupanda, kukua na kukamilika kwa kanisa. Matokeo ya kanisa linalotafuta waliopotea na kuhubiri injili ni: **makanisa mapya yanapandwa kila mahali**. Mtindo wa Kuwapeleka watu mahali Fulani kuhudhuria kanisa badala ya kupanda makanisa nyumbani ni kinyume na Injili kuhubiriwa katika kila watu katika jamii. Watu wanaliona kanisa kama kitu ambacho hutendeka mahali Fulani na kwa hivyo haliwafai. Mpaka kanisa lipandwe kila mahali ushuhuda wa injili utakuwa haujakamilika.

KUJITOKEZA KWA HUDUMA MPYA

Hatua ya SABA katika kuendeleza huduma inayofaa katika kutimiza Tume Kuu ni
kujitokeza kwa huduma mpya

Kanisa linapoendelea kutembea katika huduma za Agano Jipya, kudumu katika upendo wa Kwanza na kutenda matendo ya kwanza, Bwana akizidisha kanisa na wale waliokuwa wakiokoka.

Kila mtakatifu, kwa kawaida na kwa njia ya Mungu katika Bwana, atakua na kuwa mtenda kazi. Wengine watachipuka kama mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji na waalimu. (**Efe.4:11**), na wengine katika karama zingine kama zile za **1 Kor.12:28.** Jukumu kubwa ni kujitokeza kwa huduma za utume katika kanisa na kukuza mchipuko wa huduma mpya ambazo zitafanya kazi na wazee kutuma na kuziweka hizo huduma mahali pake katika Mwili wa Kristo.

KIZAZI KIPYA CHA WAHUDUMU

Kanisa linapoendelea kutembea katika huduma na kuwatuma wahudumu, makanisa mapya yatapandwa. Hatua inayofuata, wakati kikundi Fulani kimeokoka katika kijiji Fulani, ni **"kutawaza wazee"**. Hii inahuzisha kuandaa huduma mbali mbali katika kanisa na kufanya uinjilisti katika maeneo hayo. Wanafunzi wanapo toka na kuanza kufanya kazi ya huduma, karama Fulani na huduma Fulani Fulani zinaanza kujitokeza na kutambulika wanapoendelea kufanya kazi. Kizazi kipya cha mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji na waalimu, watenda miujiza, waponyaji, maongozi, masaidiano na kila kipawa ambacho kimepeanwa katika Agano Jipya, kitakua. Kazi ya huduma za Kristo aliyepaa inakamilika wakati Mwili wote unatenda kazi na kila kiungo kinafaidi Mwili.

NCHI YOTE ITAJAA UTUKUFU WAKE

Mwa.1:28 ***"Mungu akawabariki, na Mungu akawaambia, zaeni mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha, mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi."***

Tume Kuu ambayo Yesu alitupatia ya kuihubiri Injili kwa kila mtu na kuwafanya mataifa kuwa wanafunzi ni kazi ya mwisho ya kukamilisha lile Jukumu La Uumbaji Adamu alipewa na Mungu. Ni kupitia kwa kanisa dunia itajaa utukufu wa BWANA (**Hesabu.14:21**). Ni kwa njia ya kuhubiri na kufundisha Injili ya Bwana Yesu Kristo ndipo ***"dunia itajazwa na maarifa ya utukufu wa BWANA, kama maji yaifunikavyo bahari"*** **Habakuki.2:14**.

Wakati wawili ama watatu wanapokutanika katika Jina la Bwana na waanze kuomba katika makubaliano, watazaa matunda – nafsi zitaongezeka.

Injili inapohubiriwa nyumba kwa nyumba na makanisa yanapandwa kuwapokea waliopotea katika kila sehemu, kutakuwa na maongezeko.

Kama vile ambavyo huduma tano zinapoendelea kutenda kazi katika neema ya Bwana Wetu Yesu Kristo, utukufu wa BWANA utaonekana juu ya kanisa na nchi itajazwa pia.